JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI

Simu: +255 22 2127384
Nukushi: +255 22 2127384
Tovuti: www.osg.go.tz
Barua Pepe: info@osg.go.tz

S.L.P 71554
10 Barabara ya Kivukoni
11405 Dar es Salaam
TANZANIA

# *MAHAKAMA YATOA MAAMUZI KUHUSU UHALALI WA UWEPO WA PORI LA AKIBA LA POLOLETI, WILAYA YA NGORONGORO, ARUSHA*

Mnamo tarehe 19 Septemba, 2023; Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Arusha mbele ya Mhe. Jaji J.C. Tiganga ilitoa uamuzi katika shauri Namba 21 la Mwaka 2022 baina *Ndalamia Partareto Taiwap na Wenzake Wanne (4)* dhidi ya *Waziri wa Maliasili na Utalii & Mwanasheria Mkuu wa Serikali.*

Waleta maombi katika Shauri hili ni wananchi wakazi wa Tarafa za Loliondo na Sale, Wilaya ya Ngorongoro, Mkoa wa Arusha. Kiini cha mgogoro huu ni madai ya wananchi hao kuondolewa katika eneo lililokuwa Pori Tengefu la Pololeti *(Pololeti Game Controlled Area)* lililoanzishwa kupitia Tangazo la Serikali Na. 421 la tarehe 17 Juni 2022 (**Wildlife Conservation (Pololeti Controlled Area) (Declaration Order), 2022***)* lilitolewa na Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii. Wananchi hao wanadai kuwa walikuwa wamiliki halali wa eneo husika kabla ya kutangazwa kuwa Pori Tengefu mwaka 2022.

Aidha, mnamo tarehe 14 Oktoba, 2022, Pori hilo la Pololeti lilipandishwa hadhi na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Pori la Akiba yaani **Wildlife Conservation (Pololeti Game Reserve) (Declaration) Order, 2022** kupitia Tangazo la Serikali Na. 604 la 2022

Katika maombi yao Mahakamani, waleta maombi waliomba Mahakama itoe amri ya kumzuia Waziri wa Maliasili na Utalii kuwaondoa waleta maombi na wakazi wa vijiji 14 kwenye eneo la kilometa za mraba 1,500 zinazotengeneza Pori la Akiba la Pololeti.

Ikumbukwe kuwa tarehe 22 Agosti, 2023; Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Arusha mbele ya Mhe. Jaji D. C. Kamuzora ilitoa uamuzi wake katika maombi Na. 178 ya Mwaka 2022 yaliyofunguliwa na Latan'gamwaki Ndwati na

wenzake 6 wakiomba Mahakama itoe idhini (leave) ya kufungua shauri la kupinga Tamko ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la kuanzisha Pori la Akiba Pololeti, 2022 (Pololeti Game Reserve Declaration Order) G.N No. 604 of 2022. Mhakama katika uamuzi wake iliamua yafuatayo:

i. Ilitoa idhini (leave) kwa waleta maombi kufungua shauri la kupinga utekelezaji wa Tangazo Na. 604 la mwaka 2022; na
ii. Ilisitisha utekelezaji wa Tangazo Na. 604 la mwaka 2022 mpaka usikilizwaji wa kesi ya msingi utakapo kamilika.

Tayari wadai wamefungua maombi ya marejeo ya Kimahakama (judicial review) Na. 18 ya Mwaka 2023 katika Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Arusha ambayo yako katika hatua ya usikilizwaji.

Katika uamuzi wake, ***Mahakama imetupilia maombi hayo ya waleta maombi na kubainisha kwamba Tangazo Na.421 la mwaka 2022 lililotolewa na Waziri wa Maliasili na Utalii halipo tena katika macho ya sheria kwa kuwa tayari Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amelipandisha hadhi eneo hilo kuwa Pori la Akiba (Game Reserve, GR), kupitia Tangazo Na. 604 la mwaka 2022 na hivyo hakutakuwa na maamuzi yatakayokuwa na nguvu dhidi ya Tangazo hilo kwa kuwa halipo tena.***
***Aidha, Mahakama katika uchambuzi wa hoja zilizokuwa mbele yake ilibaini kwamba eneo ambapo Pori hilo lipo lilikuwepo tangu mwaka 1951. Hivyo, Vijiji viliposajiliwa vililikuta tayari limeanzishwa kama Pori Tengefu ambalo lilijulikana kama Loliondo Game Controlled Area na hoja kwamba eneo hilo ni ardhi ya kijiji moja kwa moja (exclusive) sio kweli bali vijiji ndivyo vilikuta Pori hilo Tengefu. Hoja nyingine tisa (9) za waleta maombi zilitupiliwa mbali na Mahakama kwa kuwa hazikuwa na mashiko kisheria.***

Maamuzi haya ya Mahakama katika shauri Namba 21 la Mwaka 2022 yakisomwa kwa pamoja na maamuzi katika maombi Na 178 ya Mwaka 2022 yana maana ifuatayo:

(i) Tangazo Na.421 la mwaka 2022 la kuanzisha Pori Tengefu la Pololeti halipo tena katika macho ya sheria kwa kuwa tayari Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania amelipandisha hadhi eneo hilo kuwa Pori la Akiba;

(ii) Mahakama imesitisha utekelezaji Tamko la Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania kupitia Tangazo Na. 604 la mwaka 2022 la kuanzisha Pori la Akiba la Pololeti mpaka usikilizwaji wa kesi ya msingi Na. 18 ya Mwaka 2023 utakapo kamilika;

(iii) Usitishwaji wa utekelezaji wa Tangazo Na. 604 la mwaka 2022, unawahusu waleta maombi katika shauri Na. 178 la Mwaka 2022 na haiwahusu watu wengine;

***(iv) Kwa kuwa Tangazo Na. 421 la mwaka 2022 la kuanzisha Pori Tengefu la Pololeti halipo tena na Mahakama imesitisha utekelezaji wa Tangazo Na. 604 la mwaka 2022 la kuanzisha Pori la Akiba la Pololeti, hali ilivyo kwa sasa (status quo) wakati ukisubiriwa uamuzi wa Mahakama katika kesi ya msingi Na. 18 ya Mwaka 2023 ni kwamba eneo lenye mgogoro linaendelea kuwa Pori Tengefu hali iliyokuwa nayo kabla ya kupandishwa hadhi kuwa Pori la Akiba mpaka Mahakama itakapotoa uamuzi kwenye Shauri la msingi. Kwa msingi huo masharti yote yanayosimamia mapori tengefu yanafuatwa ikiwemo kuomba kibali kwa Mkurugenzi wa Wanyapori ili kulisha mifugo katika eneo la Pori Tengefu kwa mujibu wa kifungu cha 21 cha Sheria ya Wanyama Pori, Sura ya 283 Juzuu la Marejeo ya 2022.***

(v) Wananchi na wadau wote wa Sekta ya Maliasili na Utalii wanakumbushwa kuzingatia sheria katika utekelezaji wa shughuli zao.

Imetolewa na:

Prisca J. Ulomi
**Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**
Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali
04 Oktoba, 2023